# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barabara ya Kilimatinde Cheyo,
S.L.P. 1020,
45112 TABORA,
Barua Pepe: rbctabora@pccb.go.tz.
**TANZANIA.**
www.pccb.go.tz

**TABORA – Aprili, 2022**

## TAKUKURU TABORA YAELIMISHA KAMATI ZA USIMAMIZI WA MIRADI ILI KUDHIBITI RUSHWA

TAKUKURU Mkoa wa Tabora kwa kipindi cha Januari 2022 hadi Machi 2022 imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na 11/2007 kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 7.
Utekelezaji wa majukumu hayo umefanyika kwa kuendelea kufanyia kazi malengo tuliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2021/2022 katika madawati ya Uzuiaji Rushwa, Elimu Kwa Umma pamoja na Uchunguzi.

### UZUIAJI RUSHWA

Dawati la uzuiaji rushwa lina majukumu makuu mawili ambayo ni ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa mifumo. Majukumu yote haya mawili yana lengo la kuweza kubaini uwepo wa viashiria au vitendo vya rushwa ili kuweza kuchunguza au kushauri mamlaka husika namna bora ya kuziba mianya ya rushwa.

Katika kipindi cha Januari – Machi, 2022 TAKUKURU Mkoa wa Tabora imefanya kazi zifuatazo:

- ✓ Uchambuzi wa Mfumo wa Utendaji wa Kazi wa Wakala wa Ufundi wa Umeme Tanzania – Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Sendees Agency (TEMESA). Katika Uchambuzi huo Yaliyobainika katika ni pamoja na

- Uwepo wa changamoto mbalimbali ambazo TEMESA wanazipata katika utendaji kazi wao kama Upungufu wa watumishi , Ucheleweshaji wa malipo pamoja na Uchakavu wa Teknoloojia

Pia warsha nne (4) zimefanyika zikiwa na lengo la kujadiliana kuhusu namna bora ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainika wakati wa uchambuzi wa mifumo kama ifuatavyo:

- ✓ Warsha ya Wadau ya Uchambuzi wa Mfumo Kubaini viashiria vya rushwa ya ngono katika Sekta ya Elimu
- ✓ Warsha ya Wadau ya Uchambuzi wa Usimamizi wa mitihani katika Vyuo vya Kati.
- ✓ Warsha ya Uchambuzi wa Mfumo wa Utendaji kazi wa Wakala wa Manunuzi wa Serikali (GPSA)
- ✓ Warsha ya Uchambuzi wa Mfumo wa Utendaji kazi wa TEMESA

## UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

TAKUKURU Mkoa wa Tabora imefuatilia jumla ya **miradi 22 ya maenedeleo** yenye thamani ya shilingi 10,171,604,327/- katika sekta za Afya, Barabara na Elimu ambayo kati yake miradi 12 yenye thamani ya shilingi 6,985,821,509.73 ilikutwa na kasoro mbali mbali ikiwemo:

- ✓ Ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma katika usambazaji wa Nukuu za bei [Quotation forms], ambapo zipo nukuu za bei ambazo zimejazwa na mtu mmoja lakini mihuri ni ya maduka tofauti na zingine imethibitika kuwa zimeghushiwa saini.
- ✓ Uchelewaji wa kuanza kwa mradi jambo ambalo linaashiria mradi kuchelewa kukamilika kwa wakati.
- ✓ Mradi kukwama kuendelea kutokana na changamoto za ubovu wa barabara kukwamisha usafirishaji wa vifaa (Mradi wa Usenye Sekondari).

- ✓ Utunzaji mbovu wa kumbukumbu za vifaa vilivyonunuliwa na vilivyotumika.

Baada ya kubaini kasoro hizo kwenye miradi husika hatua mbali mbali zilichukuliwa ikiwemo kutoa elimu kwa **KAMATI ZA USIMAMIZI WA MIRADI** waliopewa jukumu la kusimamia miradi hiyo ambayo elimu pia ilihusisha kupata ushauri wa kitaalam kuhusiana na ujenzi huo pamoja mianya ya rushwa inayoweza kujitokeza na jinsi ya kukabiliana nayo. Pia uchunguzi umeanzishwa kwa baadhi ya miradi yenye kasoro iliyouwa na dalili za kuwa na ubadhirifu wa fedha za miradi hiyo.

**ELIMU KWA UMMA**

Katika upande wa kuelimisha jamii ili ishiriki kivitendo katika mapambano dhidi ya rushwa, elimu ilitolewa kwa makundi mbalimbali ikiwemo klabu za wapinga rushwa katika shule za msingi, sekondari na vyuo, watumishi wa umma na mashirika ya Serikali. Kazi nyingine ni kama ifuatavyo:

- Semina **47,**
- Uandaaji wa makala **15**,
- Mikutano ya hadhara na mijadala ya wazi **23,**
- Utoaji wa habari na vipindi redioni **02.**
- Kuimarisha na kufungua klabu za wapinga rushwa **104.**
- Maonesho 5 yalifanyika.

**USHIRIKI WA TAKUKURU KATIKA MAADHIMISHO**

TAKUKURU (M) Tabora ilishiriki kwenye maadhimisho ya Wiki ya Sheria – Februari 2022 pamoja na Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, 2022 kwa njia ya kuweka mabanda ya maonesho ambapo wananchi walitembelea mabada haya na kuelimishwa.

**UELIMISHAJI KUPITIA TAKUSKA**

Elimu imeendelea kutolewa kwa makundi mbalimbali na wadau kupitia ushirikiano wa TAKUKURU na Chama cha Skauti (TAKUSKA), kama ifuatavyo:

- Utambulisho wa Mwongozo kwa Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari

- Kutoa elimu kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi na maafisa Elimu Kata juu ya mpango wa TAKUSKA.
- Kutoa elimu kwa Walezi wa Skauti na Skauti Mashuleni kuhusu umuhimu wa kutoa taarifa za vitendo vya Rushwa kwenye miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao.
- Kutoa elimu kwa vijana wa skauti katika makambi yao.
- Kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa skauti wakati wa maadhimisho ya kuzaliwa muasisi wa Skauti Duniani
- Kutoa elimu wakati wa sherehe za kukaribisha skauti wapya mashuleni.
- Kuanzishwa kwa Group la Whatsapp la waalimu walezi wa skauti mashuleni, maafisa elimu pamoja na maafisa TAKUKURU

**TAKUKURU INAYOTEMBEA**

Pia shughuli za uelimishaji zimeendelea kutolewa kupitia TAKUKURU INAYOTEMBEA. Kwa kipindi cha Januari - Machi 2022 TAKUKURU INAYOTEMBEA imefikia jumla ya kata mbili, ambapo wananchi walipewa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa , walitoa kero zao na baadhi zilipatiwa majibu papo kwa papo na nyingine zilipelekwa kwenye mamlaka husika ili zipatiwe majibu.

**UCHUNGUZI NA MASHTAKA**

Katika kipindi husika, TAKUKURU Mkoa wa Tabora imepokea jumla ya **malalamiko 42** ambayo kati yake **24** yalikua na viashiria vya Rushwa, na **18** hayakua na viashiria vya Rushwa. Malalamiko 24 yaliyokuwa na viashiria vya rushwa yamefanyiwa uchunguzi ambapo kati ya hayo, malalamiko 11 yako katika uchunguzi wa kina na kukusanya ushahidi wa kutosha wa kuthibitisha tuhuma za rushwa. Majalada 13 yanaendelea na uchunguzi wa awali.

**Malalamiko 42 yaliyopokelewa yalihusu sekta zifuatazo.**

TAMISEMI – 23; Afya – 7; Polisi – 6; Mahakama – 3; Ujenzi – 2 na
Binafsi – 1.

**Malalamiko 18** ambayo hayakuhusu rushwa walalamikaji 12 walipewa ushauri na malalamiko 06 yalihamishiwa kwenye idara zingine kwa ufatiliaji zaidi.

- Majalada ya uchunguzi saba (07) yamekamilika kwa ajili ya kuombewa kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani toka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Tumefungua kesi mpya mbili (2) Mahakamani. Majalada matatu (2) yalipata kibali cha DPP. Kesi mbili (2) zimetolewa maamuzi ambapo moja Imeshinda na moja imeshindwa. Jumla ya mashauri kumi na tisa (19) yanaendelea mahakamani

**MIKAKATI YA APRILI - JUNI 2022**

TAKUKURU Mkoa wa Tabora itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na kushirikiana  na wadau mbalimbali katika mapambano dhidi ya Rushwa. Tutajikita katika KUZUIA RUSHWA kwa kutoa elimu ya kutosha kwa taasisi mbalimbali na jamii ili kuhakikisha wananchi sio tu wanaifahamu na kuichukia Rushwa bali kuongeza mwamko wao katika kutoa Taarifa za vitendo vya Rushwa vinavyojitokeza katika mazingira yao.

Pia TAKUKURU (M) Tabora itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika mapambando dhidi ya Rushwa kwa kushughulikia Taarifa zinazowasilishwa kwa wakati na weledi wa hali ya juu na kutoa elimu ya kutosha kwa jamii ya mkoa wa Tabora.

**WITO KWA WAKAZI WA MKOA WA TABORA**

Natoa wito kwa wakazi wa mkoa wa Tabora kutokuvumilia uvunjifu wa maadili na vitendo vya Rushwa katika mazingira yao. Waendelee kuleta Taarifa za matukio hayo na sisi tunaahidi kuzifanyia kazi kwa usiri na weledi wa hali ya juu. Taarifa hizo zitashugulikiwa kwa usiri mkubwa na yeyote atakayedhihirika kumtisha mtoa Taarifa au shahidi aliyewasilisha Taarifa TAKUKURU hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Imetolewa na

Musa O. Chaulo
Mkuu wa TAKUKURU
**Mkoa wa Tabora**